# Living Stone Boys' Seminary (LSBS)

**0717635270/0652393337**


P.O. BOX 100 MUHEZA, TANGA

**www.lsbs.ac.tzwww.facebook.com/LSBSTZE-Mail: info@lsbs.ac.tz**


**MZAZI WA ______________________________________________**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2026 LIVING STONE BOYS' SEMINARY**

Ni neema ya ajabu kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule yetu ya sekondari kidato cha kwanza mwaka wa 2026. Tunampongeza sana. Shule yetu iko kilomita mbili (2) kutoka Muheza Mjini (stendi) eneo la Sega Mkoa wa Tanga.




Living Stone Boys' Seminary ni shule ya Bweni ya wavulana tu, inayoendeshwa kwa maadili ya Kikristo na ya Kibiblia, ingawa tunapokea wanafunzi kutoka madhehebu yote na dini zote, utaratibu wa kuabudu na uadilifu unafuata mafundisho ya kibiblia, wazazi na wanafunzi wanapaswa kulijua hili mapema, kuheshimu na kukubaliana na utaratibu huo, ambao kwa uzoefu wetu haujawahi kuleta athari wala hauna lengo la kuharibu umoja wa kitaifa.

Shule inafuata mtaala wa Elimu wa wizara ya Elimu wa Tanzania katika michepuo ya Sayansi na Sayansi ya Jamii, Shule inazingatia nadharia na vitendo katika mafunzo.

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule hii anapaswa kuzingatia yafuatayo: -

1. Mzazi/Mlezi atapaswa wakati wote kusaidiana na uongozi wa shule katika malezi ya mwanafunzi na mafanikio makubwa kitaaluma. Hivyo kila mzazi atasaini katika karatasi itakayoambatanishwa na kukubali kutoa msaada kila itakapobidi.

2. **MUDA WA KURIPOTI SHULENI**

   Shule itafunguliwa **10/01/2026** Wanafuzi wote wanapaswa kuripoti shuleni siku hiyo kuanzia saa **3:00 asubuhi** (saa tatu) mpaka **saa 11:00** jioni (kumi na moja)

**MALIPO YA ADA YA SHULE KWA MWAKA 2026**

| | ITEMS | 1ST QUARTER | 2ND QUARTER | 3RD QUARTER | 4TH QUARTER | SUB-SUM |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TUITION | 235,000 | 235,000 | 235,000 | 235,000 | 940,000 |
| 2 | BOARDING (DORM&FOOD) | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 450,000 | 1,800,000 |
| 3 | MEDICAL/EMERGENCY | 50,000 | 50000 | 50000 | 50000 | 200,000 |
| 4 | EX-CURRICULAR | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 200,000 |
| 5 | EXAMS | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 200,000 |
| 6 | LABS (PRACTICAL), COMPUTER & LIBRARY | 35,000 | 35,000 | 35,000 | 35,000 | 140,000 |
| SUM | | **870,000** | **870,000** | **870,000** | **870,000** | **3,480,000** |

**REGISTRATION FEE: 155,000/= TO BE PAID BEFORE ADMISSION TIME**

## TARATIBU ZA MALIPO

Malipo yote yafanyike kupitia benki ya NMB katika tawi lolote lililoidhinishwa na benki hiyo na risiti ya benki (Bank pay in slip) iwakilishwe shuleni wakati wa ufunguzi na usajili kwa kila muhula. Kumbuka kuwa hakuna malipo yatakayorejeshwa mara baada ya kuingiza fedha hiyo bank kwa msingi huo unapaswa kufikiri zaidi kabla ya kufanya malipo ya fedha benki.

**NB**,
Malipo yote yafanyike kupitia Benki katika Akaunti ifuatayo:

NMB – namba ya Akaunti: **41710053802**
Jina la Akaunti: LIVING STONE BOYS` SEMINARY,
Fedha za Dharura (**POCKET MONEY ZISIINGIZWE BENKI)** ziletwe kama keshi (cash). Wakati wa kuingiza malipo Benki hakikisha kuwa unaandika **Jina la Mwanafunzi**

KARIBU SANA LIVING STONE BOYS' SEMINARY.

WILLIAM JACKSON MASALA

MKUU WA SHULE